**Mt. Marko Mwinjili na Msimamizi wa Parokia**
*Aliishi Yerusalemu. Baada ya ubatizo wake, akafuatana na Mtume Paulo. Kisha aliishi Roma na Mt. Petro, akaandika Injili akikusanya mafundisho yake. Akaeneza Ukristu na kuanzisha Kanisa Aleksandria ya Misri. Akawa Mhubiri, Askofu na Shahidi wa kwanza kwenye bara la Afrika.*

**Gazeti la Parokia Katoliki**
**ya Mtakatifu Marko Mwinjili ya Ol Moran**
*N. 83 — Mwaka wa 13*
**Desemba 2021**

# SAUTI *ya Mtakatifu* MARKO

*Baada ya miezi minne usalama haujarudi kabisa: bado kuna kazi ya kufanya*

## Nini imesababisha hayo yote?

Usalama umerudi Ol Moran? Mara nyingi naulizwa swali hili. Nijibu vipi?

Tunajua matukio ya miezi iliyopita. Mwanzo wa Septemba ulileta taabu: vikundi vya majangili vilishambulia vijiji kadhaa, vikalazimisha watu kuhama. Wengine waliibiwa mali, wengine walichomelewa nyumba, wakajeruhiwa au kuuawa, kunao waliokufa kwa sababu ya mshtuko, shule zikafungwa. Wafugaji haramu wakajaa katika shamba la Laikipia Nature Conservancy, tena wakaingia kwenye mashamba ya wakulima, mavuno mengi yakaharibiwa. Eneo likarudi gizani, tukiona tena mambo ambayo tulitaka kusahau: ukabila, risasi, uuaji, wizi, hofu, chuki, kilio, vita, moto. Ol Moran na Laikipia zilitajwa kwa vyombo vya habari za kitaifa kila siku, tukirudishiwa ile sifa mbaya ya eneo bila usalama wala matumaini. Kwa sababu gani? Nini imesababisha hayo yote? Hatuwezi kuhepa swali hilo.

Bila shaka yaliyotendeka wakati huu si kwa ule mvutano wa kawaida kati ya wakulima na wafugaji. Zimetajwa sababu mbalimbali: ukame wa kaskazini umesukuma wafugaji upande huu na nyasi ni chache; uchaguzi wa kitaifa unakaribia na kuna viongozi wanaocheza siasa mbaya; wakubwa wengine wanatamani shamba la Laikipia Nature Conservancy na mashamba ya eneo hili; wengine wafaidika na mifugo haramu au katika soko la silaha, na wanatumia wafugaji kwa faida yao. Labda ni sababu hizi zote pamoja: lakini ni wazi kuwa vita hivi havileti faida kwa jamii.

> Mbona hatuwezi kuona maamuzi yanayosaidia jamii kwa jumla, wala si wajanja wachache?

Na saa hii kuko vipi? Baada ya mambo ya dharura, Serikali ilijaribu kurudisha usalama. Kunayo yametendeka: iliundwa Kirima Sub-County, sasa Ol Moran kuna DCC, kuna OCPD, barabara zinatengenezwa, maofisa wa usalama wameongezeka. Raia wa kawaida akapata matarajio makubwa sana. Hata hivyo, watu hawalali bado.

Baada ya miezi minne, bado risasi zinalia usiku, wafugaji wanakanyaga mashamba na kuvunja nyumba. Mara kwa mara wanapigana kati yao. Kila juma kuna mambo.

Kunyang'anya bunduki ni kama hakuwezekani. Mimi siwezi kutembea na silaha, lakini anayeingia shambani mwangu haulizwi, bali hubembelezwa: tafadhali lisha nyasi tu, usisumbue wenyewe! Kwani Serikali imeshindwa? Ama kuna faida ya wachache inayotunzwa kuliko uhai na mali ya wananchi? Hiyo ndiyo shida! Mbona hatuwezi kuona maamuzi yanayosaidia jamii kwa jumla, wakulima kwa wafugaji, wala si wajanja wachache?

Neno la mwisho. Je, viongozi wa siasa wamepotelea wapi? Hawawezi kutetea zaidi haki za wananchi? Saa hii wamenyamaza wote. Sijui watakuja kusema nini wakati watakapotafuta kura yetu: kwamba walituletea unga wakati wa vita?

Fr. Giacomo Basso - *Baba Paroko*

Vyombo vya habari vikitangaza taabu za eneo.






### NOELI YA AMANI NA YA HURUMA

*Tunakaribia sana sherehe ya Kuzaliwa kwake Bwana Yesu na sikukuu zinazofuata. Wakristu hufurahia kuzaliwa Mkombozi, aliyekuja kuleta nuru ya amani duniani humu.*

*Wakati huu wa Noeli tutapatana hata katika familia zetu: uwe wakati wa amani na furaha. Na tukumbuke pia wale walio na mahitaji mbalimbali.*

*Katika Makanisa tunatengeneza* ***Hori la Noeli (The Crib)****: hapo tunatoa sadaka ya Hori ambayo ni kwa ajili ya matendo ya huruma ya Parokia.*









*Matukio ya Septemba 2021*

# Ili tusiyasahau, ili tusiyarudie

Hii ni kumbukumbu fupi ya matukio makuu tangu mwanzo wa mwezi wa sita, usalama ulipoharibika katika eneo la Ol Moran. Bila shaka, kunayo mengine ambayo hayajaandikwa hapa, lakini walau haya twaweza kuyakumbuka.

*Jumanne 31 Agosti* - Majabmbazi walikamatwa sokoni Ol Moran. Wafanyabiashara walitekwa nyara sokoni Amaya (hadi siku ya leo hatima yao haijajulikana). Wasiwasi ukaanza. Wanafunzi wa jamii za Wapokot na Wasamburu walitolewa katika shule zote za eneo.

*Jumatano 1 Septemba* - Mashambulio na mauaji yakaanza. Wenyeji wa vijiji kadhaa wakaanza kuhama, vile vile wakulima walitoka mashambani mwao, hasa katika maeneo ya Miharati, Merigwit, Kahuho, Ngare Narok, Mutaro, Milango. Watu wengi wakatafuta makao kijijini Ol Moran, Survey na Ol Motunyi. Wakimbizi wengi wakakaribishwa pia Parokiani, na katika makanisa mengine (Deliverance, Baptist), na kwenye Polytechnic ya Ol Moran.

*Jumanne 2 Septemba* - Milango: Martha Muthoni Gakuru, umri wa miaka 12, mwanafunzi wa darasa la 8, alipigwa risasi kwa mguu. Ngare Narok: bw. Karigwi Gitumbo Ndung'u aliuawa; nyumba ya mzee James Ereng' ikachomwa. Mbombo: Mzee Nash Atan aliibiwa mifugo. Ratia Farm: mlinzi Rasta aliuawa. Ol Moran: Bibi wa Chief Kalenju aliibiwa mifugo. Kahuho: Jirani wa Chief Njuguna aliibiwa mifugo. Survey: Pst. Karira alishambuliwa na kuibiwa mifugo.

*Jumatano 3 Septemba* - Kisii Ndogo: Nyumba kadhaa zikachomwa.

*Alhamisi 4 Septemba* - Shule za eneo zikaanza kufungwa.

*Ijumaa 3 Septemba* - Mkutano wa RC George Natembeya kijijini Ol Moran. Nyumba nyingine zikachomwa kijijini Ngare Narok.

*Jumapili 5 Septemba* - Mirigwit: bw. Peter Kairu Njuguna aliuawa, wengine wakashambuliwa usiku.

*Jumatatu 6 Septemba* - Wenyeji wa Mirigwit na wa Ol Moran pia wakaandamana na kulalamika kwa sababu ya mauaji na usalama kuharibika.

*Jumanne 7 Septemba* - Mkutano wa RC Natembeya kijijini Ol Moran, katika Red Cross. Darasa moja la shule ya Merigwit ikachomeka.

*Ijumaa 10 Septemba* - Baraza la Minister Matiang'i kijijini Ol Moran. Alitangaza mipango ya kurudishia usalama, kufungua shule zote kuanzia Jumatatu 13 Septemba, pia mabadiliko katika eneo (Kirima Sub County mpya, OCPD na DCC wa Ol Moran).

*Jumapili 12 Septemba* - Misa ya Askofu Joseph Mbatia kanisani Ol Moran. Hata Governor Ndiritu Muriithi alihudhuria ibada na kuwaongelesha washirika.

*Jumatatu 13 Septemba* - Shule zilifunguliwa tena.

*Jumanne 14 Septemba* - Tumaini Academy ilifunguliwa. Fujo kijijini Rumuruti.

*Jumatano 15 Septemba* - Majambazi walipiga risasi karibu na Tumaini Academy saa kumi na moja jioni. Shule ikafungwa tena, wanafunzi wakahamishwa tena Parokiani. Masomo yakaendelea Parokiani hadi mwisho wa muhula.

*Alhamisi 30 Septemba* - NPRs wa Ngare Narok Charles Lokori na Robert Ekaran walipigwa risasi karibu na shule ya Tumaini. Bw. Robert akafariki hospitalini kesho yake.

Orodha hii ingeendelea hata kwa mwezi wa Oktoba na Novemba. Ndipo mashambulio yalitukia hata Githima, Ndonyoloip, Kabati na Wangwachi. Mashamba yalivamiwa, hasa kwenye maeneo ya Merigwit, Dam Samaki, Miharati, Ngare Narok, Kahuho. Askari wa KDF walishambuliwa Wangwachi, tena maofisa 2 wa Polisi waliuawa, 7 wakajeruhiwa katika shamba la Laikipia Nature Conservancy.

Hata majuma yaliyopita yamekuwa na ajali. Jumamosi 11 Desemba, majambazi walishambulia maboma, bw. Joseph Njuguna alijeruhiwa. Tena, Jumapili 5 Desemba kijana John Mwangi, ndugu wa Chief Wachiuri, alijeruhiwa mkono; Jumamosi 4 usiku bi. Loise Mwangi akapigwa risasi kwa miguu. Nyuma kidogo, Jumatano 29 Novemba, Chief Peter Wachiuri akapigwa kichwa na wafugaji haramu, akavunjika mkono.









*Misaada na Mambo Mapya*

## Mwanga katika giza

Pamoja na kukumbuka yale mabaya yaliyotukia, ni muhimu pia kuyatambua yale mema, yaliyo kama nuru gizani. Wakati shida ilitokea, hawakukosa walioamua kusaidia.

- Raia ambao waliwakaribisha wakimbizi nyumbani mwao.
- Masista na Wafanyakazi wa Parokia waliokaribisha wakimbizi na wanafunzi, na kuwatunza Parokiani.
- Wachungaji na Wakristu wa Madhehebu mbalimbali waliowatunza wakimbizi, kama Kanisa la Deliverance, Baptist, na mengine.
- Parokia mbalimbali za Jimbo Katoliki la Nyahururu, pamoja na Askofu Joseph, tena Wakristu waliojitolea na mali na misaada yao.
- Vile vile, Wachungaji na Washirika wa Makanisa mbalimbali kutoka nje waliowatembelea watu wetu, kuwaombea na kuwasaidia.
- Wasaidizi wote waliochangia pesa kwa njia ya Paybill ya Parokia #olmoran21.
- Serikali ya Laikipia County, viongozi na wafanyakazi walioleta msaada mkubwa wa vifaa na chakula, kuwatembelea watu kila siku, pamoja na Governor Ndiritu Muriithi aliyeshinda Ol Moran siku kadhaa kuongoza kazi ya kaunti.
- Mashirika yaliyokuja kusaidia kwa njia mbalimbali, hasa Kenya Red Cross, Saint Martin CSA, Caritas Nyahururu.
- Serikali za Kaunti jirani, pia Viongozi wa Serikali na Wanasiasa waliosaidia kwa ukarimu na vifaa na chakula.
- Wafanyakazi wa Parokia na Wafadhili waliochangia mradi wa Food for Work uliofanyika kule Ngare Narok.
- Viongozi na Maofisa wa Usalama, hasa Jeshi (KDF), Polisi wa Ol Moran, na kwa njia ya pekee NPRs wote wa eneo letu wanaoendelea kuwatunza wenyeji.







***GOVERNMENT INTERVENTION***

***Administration & Security***

- *New Kirima Sub-County (from Ng'arua to Lounyek).*
- *New KDF / Army camps (Merigwit, Nagum).*
- *Upgrade of Ol Moran Police Station to Sub County Head Quarters.*
- *OCPD: Mr. Donald Seilor.*
- *New OCS: Mr. Peter Mutea.*
- *DCC: Mr. John Sepeswa Orata.*
- *ACC Ol Moran Division: Julius Mukundi Nyaga.*
- *New ACCs in the Office of DCC: Mr. Steve Ochieng' Biko and Mr. Amos Mbugua Kamau.*
- *Promotion of peace-building meetings.*

***Main Structures & Infrastructures***

- *Improvement of Roads network*
- *Tarmacking of Sipili-Ol Moran road.*
- *Building of Police Head Quarters facilities.*
- *Upgrade of Ol Moran Health Centre facilities.*
- *Construction of classrooms at Merigwit Primary by KDF.*
- *Building of temporary housing for affected families.*












*Shule kadhaa zimeadhiriwa, hasara ni ya wanafunzi*

## Elimu huandamana na Amani

Wakati wa vita, mwezi wa tisa, zilifungwa Shule za Msingi za Ol Moran, Mbombo, Milango, Merigwit, Miharati, Survey, Mutaro, Mutarakwa, Gathanji, Dam Mbili, Ndunyuriwo na Tumaini Academy, pia Shule za Upili za Ol Moran na Survey. Wanafunzi wengi walihama, bali wengine hawajarudi shuleni tangu wakati ule. Kweli vita huleta hasara, bali elimu bora huleta amani.

Shule ya Upili ya Ol Moran imejitolea kujenga bweni la wavulana, kwa ajili ya wanafunzi waliohitaji kukaa shuleni usalama ulipokosekana. Mradi ulisimamiwa na Nobelity Project na fedha ya RMI. Bweni lilifunguliwa 13 Novemba, wakisherehekea na Cultural Day tofauti ya mila katika umoja wa jamii.



## *Changamoto na Maendelo ya Tumaini*

Kama shule zote jirani, hata Shule ya Parokia Tumaini Academy imepata changamoto za kutosha kwa sababu ya ukosefu wa usalama. Hata hivyo, walimu wameweza kuendelea na masomo kwa muhula wote. Kwa siku kadhaa walihamisha wanafunzi hadi Parokiani, kisha wakarudi shuleni, na juma hili shule imefunga muhula vizuri na bila wasiwasi.

Baada ya ajali zilizotukia kijijini Ngare Narok, shule imeendelea kulindwa na Polisi na NPRs mchana na usiku. Pia usalama umeongezwa na ua jipya kuzunguka mashamba jirani ya shule, na hata barabara ya kijijini inatarajiwa kutengenezwa.

Kazi ya ujenzi pia haijasimama: bweni la wavulana na ukumbi mkuu unaendelea vizuri. Pia, shule imeweza kununua gari lake, minibus aina ya matatu. Kwa hivyo, kuanzia Januari, wanafunzi wanaohitaji, wataweza kusafirishwa asubuhi na jioni.

*Matayarisho ya Silver Jubilee 1997—2022*

## Parokia yatimiza miaka 25

**Mwaka ujao utakuwa wakati muhimu kwa ajili ya Parokia, itakayoadhimisha miaka yake 25, iliyoanzishwa tarehe 1 Januari 1997.**

Viongozi wa Parokia (PPC, PFC, Waratibu wa Vituo na Makatekista Wakuu) walikutana Jumamosi 11 Desemba kujadiliana kuhusu mpango wa sherehe zitakazofanywa mwaka ujao kwa sababu ya 'Silver Jubilee' (yaani maadhimisho ya miaka 25 ya Parokia).

Kwa kuanzia, Jumamosi 1 Januari 2022, kanisani Ol Moran, saa tano, kutakuwa na **Misa ya kuubarikia Mwaka Mpya**, itakayohudhuriwa na wanachama wa PPC, PFC na Makatekista wote. Baadaye, Jumamosi 22 Januari, kutakuwa na **Parish Assembly ya 16** ya Viongozi wote, ndipo tutakapopata mpango kamili wa sherehe zote za Silver Jubilee. Hata hivyo, **Sherehe Kuu ya Silver Jubilee** itakuwa Jumamosi 30 Aprili, pamoja na Baba Askofu.

1997—2022 Silver Jubilee

SAINT MARK CATHOLIC PARISH - Ol Moran

*HABARI FUPI*

### Vijana

Vijana wa Parokia watakutana katika Ibada ya Misa ya Usiku wa Noeli, Ijumaa 24 Desemba, saa moja jioni.

Vijana wa Parokia zote tano za Dekania ya Ng'arua watakuwa na ziara ya Noeli Jumanne 28 Desemba, kwenda kwa Ziwa la Ol Bolosat, kule Ol Joro Orok. Mchango wa safari ni Ksh 1,000. Siku ya mwisho wa kujiandikisha kwa safari ni Siku ya Krismasi, tarehe 25 Desemba.

Pia, umeshaanza wakati wa Vijana kujiandikisha katika orodha ya Jimbo la Nyahururu kwa mwaka ujao (Registratation 2022). Kila mwanachama achangia KSh 150. Siku ya mwisho wa kujiandikisha itakuwa tarehe 31 Januari 2022.

### PMC: Mashindano ya Crib

Watoto wote wa PMC wamealikwa kuhudhuria maombi ya Novena ya Noeli makanisani kwao, ili kujitayarisha kiroho kwa ajili ya Sherehe ya Kuzaliwa kwake Yesu.

Vikundi vya PMC vya kila Kituo vitashindana katika kutengeneza mfano wa Hori la Noeli katika Makanisa yao. Mwalimu mmoja atatembelea na kukagua kila Kanisa.

Kama kila mwaka, watoto na Promoters wao watakuwa na Sherehe ya PMC pamoja na Nadhiri Jumapili ya Epifania, tarehe 2 Januari 2022, kanisani Ol Moran, kuanzia na ibada ya Misa saa tano.

*Sisters Servants of the Visitation*

## Nadhiri za Masista

***Perpetual Vows***

Masista 10 wa Shirika walifanya Nadhiri za kudumu, kule Italia, Jumanne 7 Desemba: Sr. Eveline (Cameroun), Sr. Jerioth (Sipili, Kenya), Sr. Lucy (Nyahururu, Kenya), Sr. Margaret (Masinga, Kenya), Sr. Secily (Embu, Kenya), Sr. Teresiah (Ol Moran, Kenya)

***Renewal of Temporary Vows by Junior Sisters***

Jumatano 8 Desemba, katika sherehe ya Maria Imakulata kanisani Ol Moran, Masista 6 walifanya upya Nadhiri za Mwaka: Sr. Angeline, Sr. Clemence, Sr. Esther, Sr. Jennifer, Sr. Joyce, Sr. Leonida.

***First Religious Profession of New Sisters***

Masista wapya 6 watafanya Nadhiri za kwanza Jumamosi 15 Januari, saa nne, kanisani Ol Moran, mbele ya Sista Mkuu Maddalena Ergasti. Misa itaongozwa na Baba Askofu Joseph. Watakuwa Masista Wapya Bernadette (Madagascar), Cecilia (Kenya), Maria (Slovakia), Nadia (Madagascar), Susan (Kenya), Teresiah (Kenya).

*Jimbo Katoliki la Nyahururu*

## Mwanzo wa Sinodi

Jimbo Katoliki la Nyahururu limefunga Mwaka maalum wa Mt. Yosefu, Jumamosi 4 Desemba, katika Kanisa Kuu la Nyahururu. Baba Askofu aliongoza Misa iliyohudhuriwa na Mapadri wa Jimbo, Masista na waakilishi wa Viongozi wa kila Parokia.

Siku hiyo, Askofu Joseph alifungua rasmi kipindi cha Sinodi pia, kitakachoendelea hadi mwaka 2023. Sinodi ilitangazwa na Papa Fransisko kwa ajili ya Kanisa Katoliki duniani kote, nayo ni wakati maalum wa kusali, kukutana, kujadiliana kuhusu maisha ya Kanisa.

Tarehe 8 Desemba, Sherehe ya Maria Mkingiwa Dhambi ya Asili, Jimbo lilimkumbuka Msimamizi wa Jimbo, Maria Imakulata.

Synod 2021 2023

For a synodal Church

communion | participation | mission



***Utaratibu wa Desemba 2021 na Ibada za Noeli***

*Alhamisi 16 Desemba* - ***Mwanzo wa Novena ya Noeli***
→ 4.00pm: Ol Moran (pia katika kila Kanisa Dogo saa yao), Maombi ya Novena ya Noeli, kila siku, hadi tarehe 24 Desemba.

*Jumapili 19 Desemba* - ya 4 ya Majilio *(Mk 6:30-34)*
→ Misa - 9am: Minjore, Miharati; 11am: Ol Moran, Mbombo.
→ 4.00pm: Ol Moran, Masifu ya Jioni na Baraka ya Kiekaristi

*Ijumaa 24 Desemba* - ***Vijilia ya Noeli***
→ 5.00pm: Ol Moran na Mithuri, Sakramenti ya Kitubio
→ Misa ya Usiku wa Noeli - 6pm: Mithuri (Mt. Maria Goretti Zone); 7pm: Ol Moran (Mt. Karolo Lwanga Zone).

*Jumamosi 25 Desemba* - ***Noeli: Kuzaliwa kwa Bwana***
→ Misa - 9am: Magadi (Mt. Mikaeli Zone); Nakwang (Mt. Papa Yohane Zone); 11am: Ol Moran (Mt. Karolo Lwanga Zone).
→ 4.00pm: Ol Moran, Masifu ya Jioni na Baraka ya Kiekaristi

*Jumapili 26 Desemba* - ***Familia Takatifu***
→ Misa - 7am: Kabati; 8am: Survey; 9am: Githima; 10am: Naibor; 11am: Ol Moran; 12noon: Posta.

*Jumanne 28 Desemba*
→ 6am: Ziara ya Vijana wote wa Dekania ya Ng'arua kwenda kwa Ziwa Ol Bolosat, kule Ol Joro Orok.

*Ijumaa 31 Desemba*
→ 10am: Ol Moran, Misa ya Shukrani ya mwisho wa mwaka.

*— MWAKA WA BWANA 2022 —*

*Jumamosi 1 Januari - Sherehe ya Maria Mama wa Mungu*
*- Siku ya Amani Duniani Kote*
*- Mwanzo wa Sherehe za Silver Jubilee (Miaka 25 ya Parokia)*
→ 11am: Ol Moran, Misa na Baraka ya Mwaka Mpya, pamoja na PPC, PFC na Makatekista wote
→ 11am: Ol Moran, Misa na Sherehe ya Msimamizi wa Kanisa Dogo

*Jumapili 2 Januari - Epifania (Tokeo la Bwana)*
→ Misa - 9am: Magadi, Gituamba; 11am: Miharati
→ 11am: Ol Moran, Misa na Sherehe ya PMC

SAUTI *ya Mtakatifu* MARKO

*- No. 83, Year 13, Printed on 15th December 2021 - (NOT FOR SALE)*

**SAINT MARK** CATHOLIC PARISH - Ol Moran - *Catholic Diocese of Nyahururu*

*P.O.Box 20 - 20320 Kinamba* - saintmark@olmoran.it - *+254 720 924 153*